Teacher.co.ke

102/3 MK
KCSE
KISWAHILI
KARATASI YA 3
FASIHI
MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA
Disemba 2023

Teacher.co.ke

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# KENYA CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION

KISWAHILI

KARATASI YA 3

*FASIHI*

**Mwongozo wa Kusahihishia**
**(SIRI)**

**MWONGOZO HUU WA KUSAHIHISHIA NI MILKI YA BARAZA LA MITIHANI YA KITAIFA LA KENYA (KNEC) NA SHARTI KUREJESHWA KWA BARAZA HILI BAADA YA USAHIHISHAJI.**

**Mwongozo huu wa kusahihishia una kurasa 14 zilizopigwa chapa.**

*© 2023 The Kenya National Examinations Council*



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

1. (a) (i) Elimu haina kikomo.

(ii) Wengi hawaelewi suala la elimu.

(iii) Ipo haja ya kuihamasisha jamii kuhusu elimu.

(iv) Anayepokea elimu atapata malipo mema kutoka kwa mwenyezi Mungu.

(v) Shuleni, msomi atapata maarifa mbalimbali.

(vi) Elimu ya awali ni ya nyumbani.

(vii) Elimu ina manufaa kwa anayepokea.

(viii) Elimu inaweza kutolewa kwenye miktadha ya tamaduni kama vile jando na kumbi.

(ix) Ulimwengu pia unatoa elimu/unamwelimisha mtu kupitia kwa matukio maishani kama vile kufungwa jela.

(x) Elimu inamuadilisha mtu na kumfanya mwenye thamani.

(xi) Tunapata èlimu kutokana na hali tunazokumbana nazo maishani. Kwa mfano, umuhimu wa kutia bidii maishani ili kuepuka dhiki.

(xii) Hutupatia mambo mengi

**Hoja 6 x 1 = 6**

(b) (i) tanakuzi – unapotoka – waingia. Nyumbani – shuleni – duniani.

(ii) tashihisi – utafunzwa na dunia.

**Hoja 2 x 1 = 2**

(c) (i) Shairi lina beti kumi.

(ii) Kila ubeti una mishororo minne/tarbia.

(iii) Kila mshororo una vipande viwili; ukwapi na utao-mathnawi.

(iv) Vina vya ndani na vya nje vinabadilika kutoka ubeti hadi mwingine isipokuwa mshororo wa mwisho katika kila ubeti.

(v) Shairi hili lina kibwagizo – Elimu nawambieni, kwamba haina kikomo.

(vi) Kila mshororo una mizani 16 (8, 8).

**Hoja 4 x 1 = 4**

(d) (i) Inkisari: kwiba-kuiba, kizoea – ukizoea, tabu – taabu

(ii) Tabdila: siyo – sio, muyatie – myatie, mumepata – mmepata

(iii) Kuboronga sarufi: - kama si somo semeni – semeni kama si somo

- wapi nitie mpini – nitie wapi mpini?

**Hoja 2x2=4**
**Kutaja 1**
**Ufafanuzi 1**

Taja – 4
Ufafanuzi – 1
1x2 = 2

(e) Kushauri/kuonya/kuelekeza/kukejeli/kuhimiza

**Hoja 1 x 2 = 2**

(f) **Mshairi anatufahamisha kuwa ana jambo muhimu analotaka kutuhamasisha na anahisi kwamba wengi hawalifahamu.** Kwa hivyo, **anatuomba tumpe nafasi azungumze kuhusu elimu** ambayo **haina mwisho.**

**Hoja 4 x ½ =2**

2\. (a) (i) Ni kauli ya msimulizi; Mwandishi

(ii) Kumhusu Umu.

(iii) Yumo kwenye kituo cha polisi ~~ambapo ameenda kuripoti kuhusu kupotea kwa Dick na Mwaliko~~.

(iv) Askari anamwambia arudi nyumbani watachunguza ndipo haya yanasimuliwa. anaenda kuripoti kuhusu kupotea kwa nduguze

**Hoja 4 x 1= 4**

**(Dondoo limetolewa ukurasa wa 83)**

(b) (i) Wajeuri – Wanauliza kwa nini watoto hawajaandikisha kupotea kwao kwenye OB.

(ii) Kutojali – Wanasema watoto wana tabia ya kutekwa nyara badala ya kumpa Umu matumaini.

(iii) Wenye mapuuza – Wanamwambia Umu kuwa watawajuza wazazi na hali hata hawajamuuliza kuwahusu wazazi wake.

(iv) Wadadisi – Wanamuuliza Umu maswali ya kudadisi, kwa mfano, walichovaa watoto walipoondoka.

(v) Watepetevu – Wanamwambia Umu kuhusu kuwajuza wazazi ilhali hawamuulizi majina ya wazazi wake. ingawa walijua kulikuwa na visa vya utekaji nyara wa watoto hawakuzui

(vi) Wasumbufu – Wanamuuliza Umu msururu wa maswali bila kumpa muda wa kuyajibu.

(vii) Wenye kukatiza tamaa – Kusema watoto wana mazoea ya kutoroshwa.

(viii) Waongo – walahadi kuchunguza kupotea kwa Dick na Mwaliko na kuwajuza wazazi wao matokeo yake ilhali hawakufanya hivyo.

(ix) Katili – Hawakumsaidia Umu kumpata ndugu zake licha ya umri wao mdogo.

(x) Wenye Mzaha – Wanamuuliza wakati walipopotea na walichovaa

**Hoja 6 x 1= 6**

Za kwanza 6x1 = 6



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(c)

(i) Kufutwa kwa baba yake na kuondolewa kwenye nyumba ya kampuni.

(ii) Kuhamishwa Msitu wa Mamba hadi Mlima wa Simba ambapo nyumba ni ndogo.

(iii) Kusomea katika mazingira mageni yenye baridi.

(iv) Kusomea shule za watu wa kima cha chini kiuchumi katika Mlima wa Simba.

(v) Kuachwa na mama.

(vi) Kifo cha baba.

(vii) Dhiki ya kuanza kuwahangaikia ndugu zake.

(viii) Kujipata kwenye mji asiouzoea na kuhangaika kutafuta yule ombaomba angaa amsaidie.

(ix) Kupotea/kutekwa nyara kwa Dick na Mwaliko.

(x) Kulazimika kuishi katika makao ya watoto.

(xi) Kuishi na familia geni. (upweke)

(xii) Kuishi na wasiwasi wa kutojua waliko ndugu zake.

(xiii) Dhiki za kisaikolojia baada ya kuacha na mama yao

(xiv) Kukosa upendo wa wazazi. Mama kuwaacha na baba kufa.

**Hoja 10 x 1= 10**

(Za kwanza $\frac{x}{10}$ = 10)

**Tanbihi**

**Mtahiniwa aonyeshe changamoto ambazo zinamkumba Umu.**

(xv) Umu kuhangaishwa kusumbuliwa na polisi pale kituoni

3. (i) **Wanaendeleza mauaji**

- Mama yake Sauna anamfanya Sauna kuavya mimba **(uk. 155).**
- Wanazaa watoto na kuwatupa: Immaculate anaokotwa na Neema kwenye taka.
- Huko kwenye taka pia kunapatikana vijusi vilivyotupwa.
- Wanajiua wenyewe kwa kujiingiza kwenye ulevi: Subira, mkewe Kaizari anapatikana amefia chumbani akiwa na chupa ya kinywaji kikali.

(ii) **Wanatelekeza majukumu ya malezi**

- Naomi, mama yake Umu anawaacha watoto wake kwa kutaka kukimbia umaskini.
- Subira, badala ya kutafuta mbinu za kuishi na mama mkwe, anawaacha Mwanaheri na Lime na kuhamia mjini.
- Mama yake Pete anaolewa na kumwacha; hajui anavyoendelea shuleni.
- Tindi kumwacha ndugu yake Kemi mikononi mwa wauaji
- Rehema kumtelekeza Chandachema (UK 104)

Nafasi ya mwanamke katika kutegua wa wanawake



Teacher.co.ke
For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(iii) **Wanachangia katika kuendeleza ndoa za mapema**

Mama ya Pete anashirikiana na wajomba kumwoza mapema licha ya rai ya bibi yake kwamba wamwache aendelee na masomo **(uk.148 – 149).**

(iv) **Wanaendeleza ulanguzi wa watoto/ binadamu**

Sauna anawateka nyara Dick na Mwaliko, anampeleka Dick kwa Buda. Yeye na Bi. Kangara wanawaingiza vijana katika madanguro.

(v) **Wanaendeleza ajira ya watoto**

Sauna anampeleka Dick kwa Buda ambapo anaajiriwa. Bi. Kangara ana mtandao ambapo anawapata vijana na kuwasafirisha baadhi yao ughaibuni kufanya kazi za kujidhalilisha.

(vi) **Wanachangia kusambaratika kwa asasi ya ndoa**

Mavyaa wa Subira anamsimanga Subira hadi Subira anaondoka. Naomi anamwacha Lunga, mkewe Kiriri, Annette, anamwachia mumewe upweke na kwenda ng'ambo.

(vii) **Wanawasababishia wengine dhiki za kisaikolojia**

Mkewe Kiriri anamwacha pweke na kuenda ughaibuni. Naomi anamwachia Lunga upweke hadi Lunga anaaga dunia kwa shinikizo la damu.

(viii) **Wanahatarisha afya za wengine kwa kuwauzia bidhaa duni**

Sauna anawauzia watu maji ya mto yaliyotiwa kwenye chupa za *mineral water*.

(ix) **Wanawaingiza vijana katika matumizi mabaya ya vileo**

Sauna anampeleka Dick kwa Buda ambaye anamtumia kulangua dawa. Dick analazimika kutumia dawa hizo.

(x) **Wanachangia uhamiaji ng'ambo wa nguvumali**

Sauna na Bi.Kangara wanawapeleka vijana ughaibuni wanakofanya kazi za kujidhalilisha.

(xi) **Kuwaingiza wanawake wenzao/wasichana kwenye madanguro** – Bi.Kangara na Sauna wanawauza wasichana katika madanguro.

(xii) **Kutowaambia kuhusu usuli wao**

Mama yake Kairu hamwambii Kairu baba yake hasa ni nani.

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Tete

(xiii) **Kuwapiga waume zao**

Mwanaharakati anasema kuwa mamia ya wanaume wanapigwa na wake zao na hakuna anayewatetea.

(xiv) **Kukatiza elimu ya watoto**

Mama Pete anaungana na wajomba wa Pete kumwoza kwa Fungo na kumfanya aache shule akiwa darasa la saba.

(xv) Kuwanyima ushirika na wanao - Mkewe Kiriri anahamia ng'ambo na watoto

(xvi) Wanachangia udhalilishaji kwa hadhi ya binadamu - kwa kutupa watoto - aliyeokotwa na Neema / wengine wanatupwa kwenye kituo cha Benefactor - vijusi vilivyo- tupwa kwenye taka.

**Hoja 10 x 2= 20**

**Kutaja 1**

**Ufafanuzi 1**

4. (a) (I)

(i) Anayezungumza ni Sara.

(ii) Anazungumza na Neema.

(iii) Wameketi ukumbini, nyumbani kwa Neema.

(iv) Neema anamdadisi mamake kuhusu uhusiano wake na baba yao (Yona).

**Hoja 4 x 1= 4**

Makazi - Satua

**(Dondoo limetolewa ukurasa wa 20)**

(II) Kutahadharisha/kuonya/kushauri /Kuelekeza

**Hoja 1 x 2 = 2**

Sauna (xvii) *teua *Satua (xxi)

(III) (i) Taswira hisi – umchukie kuku bure. Kuchafuka roho

(ii) Taswira muonjo – alacho kuku, hutaila (Za kwanza 2 x 1 = 2)

~~**Hoja 2 x 1 = 2**~~

(xvii) Kuwanyima watoto haki ya kuteua - uhuru wa kuamua - Mamake Sauna anamlazimisha kuavya mimba.

(xviii) Kumnyima mume haki ya unyumba / kuishi na mke - Naomi anamtoroka Lunga, Anette kumwacha Kiriri kwenda kuishi Ng'ambo

(xix) Kuwatesa watoto kwa kuwapa kazi ngumu, zahali.

(xx) Kujiingiza katika tendo la ukandamizi / hatari - Tuama

(xxi) Kuwanyima uhuru wa kusema / kupigania haki - Mamake Sauna anamwambia asimpe tope Maya.

(xxii) Kuwanyima haki ya makazi - Malalamishi ya Bi Satua kuhusu sukari, matumizi ya kihdelo ya sabuni na kubanana chumbani kwa malazi. chanda chema

(xxiii) Wanaendeleza uavyaji mimba - Mamake Sauna anamlazimisha kuavya kitoto anaondoka ukiukaji wa haki kwa kuhifadhi himaya / Pete anaenda

(xxiv) Wanasababisha mahali / vitu anayomiliki mtu - Wanawake wanaohusiana kimapenzi na Tenge wakati kimai kwake nyumbani kwake

(xxv) Sauna kuwateka nyara Dick na Mwaliko. Sauna anawaondoa Dick na Mwaliko mamake Mazingira wanayozoea - anaendeleza ubaguzi wa nduguze Kumwoza Pete kwa Fungo ili kupata pesa za kumuoa

Zozote 10 x 2 = 20



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

(IV)

(i) Kupitia kwake tunatambua suala la elimu – mhusika ana shahada mbili, amegharamia elimu ya nduguze na anathamini elimu ya wanawe.

(ii) Ametumiwa kuendeleza maudhui ya ndoa – Ameolewa na Bunju, anamhoji mamake kuhusu ndoa yake na babake.

(iii) Anaendeleza suala la uwajibikaji – Anawatunza wazazi, anawashughulikia nduguze na kuwalea wanawe.

(iv) Kupitia kwake tunatambua suala la mshikamano wa kijamii – anatangamana vizuri na wazazi, nduguze na familia yake.

(v) Anachimuza suala la mabadiliko – Amesoma, anafanya kazi, tofauti na ilivyokuwa awali.

(vi) Anaendeleza suala la malezi – Anashirikiana na mumewe kuwalea wanawe.

(vii) Anajenga mgogoro katika tamthilia:

- Mgogoro wa nafsi – Maamuzi ya Bunju (mama kutolala kwake) yanamkwaza.
- Mgogoro baina yake na Bunju – Kuhusu majukumu ya kifamilia na masuala ya utamaduni.

(viii) Anaendeleza ploti – anasafiri kwenda kijijini kumchukua mama na kumrudisha kijijini baada ya kupokea matibabu. ~~Anamsimulia Bunju kisa cha ajali~~.

(ix) Kupitia kwake tunatambua sifa za wahusika wengine – Uwajibikaji wa mamake na msimamo imara wa Bunju kuhusu masuala mbalimbali.

(x) Kupitia kwake tunatambua dhamira na falsafa ya mwandishi. Tunatambua mtazamo wa mwandishi kuhusu nafasi ya utamaduni, usawa na kijinsia.

(xi) Kupitia kwake tunatambua suala la maendeleo. Anamtanabahisha mama yake kwamba jamii nyingi zimeendelea, nao wamebaki hapo hapo.

(xii) Ametumiwa kuonyesha mikinzano ya utamaduni.

(xiii) Ametumiwa kuonyesha athari hasi za shughuli za kujiendeleza kiuchumi na kijamii (changamoto katika malezi ya wana, mtafaruku katika ndoa.)

(xiv) Kupitia kwake tunatambua suala la taasubi za kiume. Bunju anamkumbusha kuwa yeye ndiye kichwa cha familia.

(xv) Anafunza maadili kama vile upendo, unyenyekevu, uwajibikaji na bidii.

**Hoja 6 x 1 = 6**



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

(b) **Mikakati ambayo Yona na Sara wanatumia kudumisha ndoa yao**

(i) Yona anatekeleza majukumu yake; anakidhi mahitaji ya familia yake. Anawasomesha wanawe, anawachunga mifugo na kushughulikia mashamba.

(ii) Sara anatambua na kumshukuru Yona kwa kuwajibikia malezi. Anamwambia Yona kwamba aliicheza sehemu ya malezi vizuri **(uk. 2)**.

(iii) Wanashirikiana katika malezi. Yona anasema kwamba Sara alimsaidia kulea na kusomesha watoto katika kipindi kigumu. Sara akiuza maziwa na bidhaa za shambani sokoni, naye Yona akishughulikia ng'ombe na shamba. **(uk. 62)**

(iv) Sara anawajibika majukumu yake kama mke. Anaposhindwa kumpikia Yona, anamwomba Dina kuja kumsaidia.

(v) Wanahifadhiana dhidi ya shutuma za watu. Pamoja na ulevi wa Yona, Sara anamtetea mbele ya watoto wake. Anamwambia Neema kwamba baba yao alijaribu. Anamtetea kwamba aliyofanya yalitokana na midomo ya watu **(uk. 19)**. Yona naye anamtetea Sara dhidi ya lawama ya Beni, kwamba ameenda kuishi mjini na watoto. **(uk. 61 – 63)**.

(vi) Wanabuni mikakati ya kusuluhisha migogoro yao. Sara anamwambia Neema kwamba walibuni mizaha ya kufanyia matendo ya Yona ambayo yangewaponza. **(uk. 20)**. Sara anasema ilibidi ajue namna ya kuishi na mlevi wake. **(uk. 20)**.

(vii) Wanakosoana inapobidi. Yona anapolalamika kwamba Sara anamchongea kwa watoto, Sara anamwambia kuwa anayafanya makubwa **(uk. 4)**. Yona naye anamwambia asiyafanye marefu **(uk. 4)**.

(viii) Wanajenga mazoea ya kudumisha mahusiano ya kifamilia. Yona anaipikia familia yake. Awali, Yona na Sara walikuwa wakipika chakula pamoja. **(uk. 74)**.

(ix) Wanasameheana/wanahimiza maridhiano. Yona anapotambua kwamba alimkosea mkewe anaomba msamaha **(uk. 74)**.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

(x) Wanatenga nafasi ya kushughulikia masuala ya kibinafsi. Yona anamruhusu mkewe kwenda mjini kushughulikia afya yake/matibabu. Sara analiona jambo la kawaida kwa Yona kujumuika na wazee wenzake.

(xi) Maadili kama vile ustahimilivu unawafanya kuhimili udhaifu wa mwenza. Sara anajifunza kuishi na mlevi wake. Dina anamsifu Sara kwa uvumilivu wake. Hata Kiwa anaajabia tabasamu ya Sara pamoja na matatizo aliyo nayo, anasema ni mwanamke jasiri.

(xii) Thamani yao kwa watoto inawafanya kuvumiliana. Sara anasema kwamba alijua watoto si nguo ya kutungwa ilibidi ajue namna ya kuishi na mlevi wake.

(xiii) Kuwaelimisha watoto kunasaidia kuwapunguzia mizigo ya kiuchumi ambayo ingezorotesha zaidi uhusiano wao. Neema anawakimu. Anashughulikia afya yao, hata amewajengea nyumba.

(xiv) Kuwathamini wana wao. Sara anawaona watoto kama zawadi ya ushirika wake na Yona. (uk. 4)

**Hoja 6 x 1 = 6**

5. (a) **Maudhui**

(i) Suala la jinsia/ Ubaguzi wa kijinsia – Sara anatukanwa kwa kupata watoto wa kike.

(ii) Dhuluma – Sara kutukanwa kwa sababu ya kupata watoto wa kike.

(iii) Uwajibikaji – watoto wa Sara wanajiendeshea mambo yao.

(v) Imani katika dini / Dini- Sara anamshukuru Mungu kwa watoto aliompa.

(vi) Utamaduni- mtazamo wa jamii kuhusu watoto wa kike.

**(Dondoo limetolewa ukurasa wa 13)**

**3 x 1 = 3**

(ii)
- Toni ya huzuni/masikitiko: Sara anatokwa na machozi.
- Toni ya kulalamika – Sara analalamikia kutukanwa.
- Toni ya ukakamavu – Sara anafurahia hali ya watoto wake kujitegemea.

~~Ameridhika. Yu tayari hata kufa.~~

**Hoja 1 x 2 = 2**
**Kutaja – 1**
**Mfano -**



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(iii) **Mbinu za lugha**

(i) Kuzungumza moja kwa moja na msemewa – Dina nimesemwa…

(ii) Tanakuzi- faraghani – hadharani.

(iii) Tabaini – si makanisani, si magengeni.

(iv) Tasfida – hata nikiitwa – badala ya, hata nikifa.

(v) Usambamba – si makanisani, si magengeni.

(vi) Matumizi ya nafsi ya kwanza- **Mimi ni**nashukuru kwa hawa alionipa Mungu.

**Hoja 3 x 1=3**

(b)

(i) Wazazi kuwajali wana wao. Sara anamweleza Yona kuwa hafai kutarajia mengi kutoka kwa Neema kwani anashughulikia mahitaji mengi.

(ii) ~~Ujirani mwema~~. Dina anaenda nyumbani kwa Sara ~~kumjulia hali na pia~~ kumpikia chakula.

(iii) Watoto kuwashughulikia wazazi- Bunju na Neema wanawajengea wazazi wa Neema nyumba kijijini.

(iv) Ndugu kuwajali wenzao- Neema anawasomesha wanuna wake.

(v) Kujitolea katika kutekeleza majukumu- Bunju anajitolea kugharamia mahitaji yote ya nyumbani ili Neema ashughulikie mahitaji ya wazazi na wanuna wake.

(vi) Ukarimu wa majirani- Luka anawakaribisha wazee wenzake ili washiriki chakula, vinywaji na mazungumzo.

(vii) Wazazi kuwalea wana wao kwa njia inayofaa- Yona na Sara, Bunju na Neema wanatekeleza majukumu yao ya malezi ya wana kwa kuzingatia maadili.

(viii) Utu wa Bunju- Bunju kumsaidia Neema alipohusika kwenye ajali.

(ix) Upendo na ukarimu miongoni mwa wanandoa- Bunju anamnunulia Neema gari hata ingawa Neema ana kazi yenye ujira.

(x) Bunju anamtuliza Neema anapohisi kuwa amemuumiza kihisia kwa kumkumbusha wema aliomtendea.

(xi) Neema anawaajiria wazazi wake wafanyakazi.

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(xii) Sara kutomuumbua mumewe mbele ya wanawe.

(xiii) Sara kuwashauri Asna na Neema kutomhukumu Bunju.

(xiv) Sara kumwonya Asna dhidi ya kuingilia uhusiano wa Neema na Bunju.

(xv) Yona kuomba msamaha kwa familia yake.

(xvi) Luka anamwonya Beni dhidi ya kufurahia machungu ya wengine huku yeye akihisi vibaya anapotajiwa yake.

**Hoja 6x2=12**

**Kutaja 1**

**Ufafanuzi 1**

6. (a) I. (i) Msemaji ni Tembo (msimulizi).

(ii) Anamrejelea Mwanaheri katika barua yake kwa mkewe.

(iii) Yuko hospitalini.

(iv) Amemwandikia mkewe (Emmi) barua kwa usaidizi wa Salim kumjuza kuhusu yaliyomfika na kuomba msamaha. Amempagaza Mwanaheri utarishi.

**Hoja 4 x 1 = 4**

**(Dondoo limetolewa ukurasa wa 52)**

II. (i) Chuku – akili inayonata mafunzo kuliko sumaku, urembo usiomithilika – kusisitiza.

(ii) Tashihisi/uhuishaji – akili kunata – kubainisha hali katika uwasilishaji.

(iii) Taswira – Kunata kuliko sumaku, urembo usiomithilika – kubainisha uhalisia wa hali fulani.

(iv) Nahau – Akili nyepesi – kubainisha hali.

**Hoja 2 x 2 = 4**

**Kubainisha mbinu 1**

**Kueleza umuhimu 1**

III. (i) Ni karimu – Msimulizi anamshukuru kwa ukarimu wake – anaenda kumwona mgonjwa (Tembo) hospitalini na anaahidi kumpelekea mkewe barua.

(ii) Ni mwaminifu – Kuahidi msimulizi kuwa barua yake itasomwa na Emmi.



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(iii) Ni mwerevu – ana akili nyepesi masomoni, ana akili yenye kunata mafunzo kuliko sumaku.

(iv) Mwenye utu – anamtendea msimulizi wema, anathamini utu wa mtu.

(v) Ana msimamo thabiti katika maisha – Ni mja wa falsafa moja siku zote: mtu ni watu.

**Hoja 4 x 1 = 4**

(b) (i) Kufutwa kazi - Tembo anavuliwa umeneja kwa sababu ya uraibu wa pombe.

(ii) Kupoteza mali - Tembo anakiri kuwa amepoteza kila kitu alichomiliki.

(iii) Kuvurugika kwa mahusiano – Uhusiano baina ya Tembo na wazazi wake ulivurugika, dada na kaka zake walimtenga.

(iv) Fujo/vurugu/ghasia – Tembo alizusha fujo maziarani alipolewa.

(v) Aibu – Tembo anazusha fujo maziarani na kukiaibikia kitendo hicho.

(vi) Athari za kiafya – Tembo anapoteza uwezo wa kuona vizuri na anakimbizwa hospitalini.

(vii) Maafa – Baadhi ya walioshiriki unywaji pombe wanaaga dunia.

(viii) Kuteleza familia – Tembo hawajibikii familia yake.

(ix) Kujiingiza kwenye anasa – Tembo kwenda kushiriki anasa huko Majengo.

(x) Ukosefu wa Amani na utulivu katika ndoa- Tembo haelewani na mke wake Emmi kwa sababu ya ulevi.

(xi) Kiburi – Tembo kujidai bingwa wa maisha.

(xii) Dhiki za kisaikolojia – ulevi wa Tembo unamwathiri Emmi kisaikolojia.

(xiii) Majuto – Tembo anajutia vitendo vyake.

**Hoja 8 x 1 = 8**

7. (a) (i) Makazi duni- Mwakuona kuzaliwa na kulelewa katika mtaa duni wenye nyumba zisizo na thamani ya kuitwa nyumba.

(ii) Mavazi duni- Mwakuona na wenzake kuwa na uhaba wa mavazi. Wengine walivaa mararu.

(iii) Ukosefu/uhaba wa lishe: Bwana na Bi. Mtondo walijizatiti kupata angalau kibaba cha unga wa chakula kwa ajili ya wana wao. Wadogo wakafaidi, wakubwa wakaramba vyungu.

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

(iv) Utapiamlo miongoni mwa watoto – Wana wa Bwana na Bi. Mtondo walitambaliwa na utapiamlo na hali ilipokuwa mbaya zaidi, utapiamlo uligeuka unyafuzi (kwashakoo).

(v) Ukosefu wa uwezo wa kugharamia elimu- wavyele wa Mwakuona kukosa uwezo wa kugharamia elimu yake ya juu.

(vi) Ukosefu wa fedha- Wazazi wa Mwakuona kukosa uwezo wa kumpigisha picha awali (kabla ya kutoweka kwake). Wazazi wa Mwakuona kukosa pesa za 'kuwatilia askari gari mafuta'.

(vii) Maskini wanashawishika kwa wepesi – Mwakuona anashawishika na kuhadaiwa na wakala kwa sababu ya hali yake ya uhitaji.

(viii) Maskini kutumiwa vibaya / kudhulumiwa– Mwakuona alitumiwa vibaya kwenye hoteli ya *Chenga -ways*.

**Hoja 5 x 2 = 10**
**Kutaja 1**
**Mfano 1**

(b) (i) Babu Fadhumo kumtimizia mwanawe mahitaji yake yote kwa uwezo wake.

(ii) Binamu ya babake Fadhumo kumpa Fadhumo hifadhi wakati mwingine shule zilipofungwa.

(iii) Fadhumo kuwa mlezi wa nduguze baada ya wazazi wao kuaga dunia.

(iv) Mjombake Fadhumo kukubali kumlipia kakake Fadhumo karo.

(v) Mume wa Fadhumo kukubali kumsomesha nduguye Fadhumo na kuwasaidia wale wengine watatu wa kike.

(vi) Mume wa Fadhumo kukubali kugharamia elimu yake.

(vii) Mwalimu mkuu kumliwaza Fadhumo kabla ya kumjuza habari za tanzia.

(viii) Fadhumo kusitisha masomo yake japo kwa muda, na kuwapa nduguze nafasi wasome. Baadaye anarejelea kukamilisha masomo yake.

(ix) Adan kuwa na msimamo dhabiti kuhusu masomo na kufanya kazi kwa Fadhumo hata baada ya ushawishi wa mjomba.

**Hoja 5 x 2 = 10**



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

8. (a) I. Ngano/hadithi za mazimwi

2 x 1 = 2

II. (i) Taswira – Zimwi kuwa na jicho moja kipajini na jingine kisogoni.

(ii) Chuku – ~~Zimwi kuanguka kwa kishindo cha mtetemeko wa ardhi,~~ maumbile ya kiajabu ya zimwi.

(iii) Nidaa – Laiti ungeliona!

(iv) Swali la balagha – Hivi zimwi hili lilikuwa halishibi?

(v) Tashibihi – mfupi kama nyundo na mwembamba kama sindano.

(vi) Nahau – kumtia kiganjani, piga moyo konde.

(vii) Mdokezo wa methali – wenzake wameshanyolewa na sharti atie chake maji.

(viii) Uradidi – siku ya siku, moja kwa moja.

(ix) Taharuki – kitakachotokea baada ya Doti kuchonga kijiti hatukijui, tuna hamu ya kukijua.

(x) Uzungumzi nafsia – Doti kujisemea nafsini atakavyokabiliana na zimwi.

(xi) Upenyezi wa msimulizi – Laiti ungeliona!

(xii) Sitiari – moyo wa simba.

Hoja 8 x 1 = 8

(b) (i) Kuonyesha hisia usoni.

(ii) Kuuliza na kujibu maswali.

(iii) Kuimba nyimbo.

(iv) Kupiga makofi.

(v) Kutoa majibu ya methali iwapo itadokezwa na mtambaji.

(vi) Kutegua vitendawili iwapo vitategwa na mtambaji.

(vii) Kuigiza baadhi ya vitendo katika masimulizi.

(viii) Kuitamba upya ngano hiyo.

Hoja 6 x 1 = 6

(c) (i) Kuwarithisha vijana kwa kuandaa vikao vya kusimuliana ngano.

(ii) Kutumia ngano kama nyenzo za kufunzia lugha.

(iii) Kuhifadhi ngano kwenye vitabu, kanda za video na kwenye mitandao.

(iv) Kuwa na vipindi vya masimulizi ya ngano katika vyombo vya habari.

(v) Kufanyia kipera cha ngano utafiti ili kulinganisha ngano za jamii moja na nyingine.

(vi) Kuhimiza utendaji wa kipera cha ngano kupitia kwa kuandaa vikao vya masimulizi.

Hoja 4 x 1 = 4



For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

(xviii) Kushiriki kama wahusika (role playing)

(xix) Kuhifadhi kwenye kompyuta / tarakilishi / CD

For more FREE CBC/KCPE/KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/